Swahili

# Jinsi ya kupata matokeo ya kipimo chako cha COVID-19

Kuna njia tatu ambazo unaweza kupata matokeo ya kipimo chako:

1. Kupitia Msimbo wa QR wa kibinafsi
2. Kupitia Lango la Matokeo
3. Kupitia ujumbe wa SMS uliotumiwa kwa simu yako ya mkononi

**Baada ya kipimo chako, utapaswa kujitenga hadi utakapopata matokeo yako.**

- Nenda nyumbani moja kwa moja na ujitenge ila umeshauriwa tofauti na Idara ya Afya NSW.
- Kaa nyumbani hadi utakapopata matokeo yako, hata kama hujisikii kuwa mgonjwa.
- Watu wengi wanapata matokeo yao ndani ya muda wa masaa 24.

**Chaguo 1: Msimbo wa QR wa kibinafsi**
Ikiwa umepewa karatasi wakati ulipopimwa ambayo ina msimbo wa QR wa kibinafsi (pamoja na jina lako na tarehe yako ya kuzaliwa chini yake), tafadhali ichanganue msimbo ule wa QR kwa kutumia kamela ya simu yako ya mkononi na bonyeza send (tuma).

Msimbo huu wa QR una habari yako ya kibinafsi ndani yake. Hauwezi kutumiwa na mtu mwingine yeyote.

**Chaguo la 2: Lango Mtandaoni la Matokeo**
- Tembelea tovuti kwa https://my.pathology.health.nsw.gov.au
- Utaulizwa kuweka nambari ya simu yako ya mkononi halafu bonyeza kifute cha bluu. KUMBUKA kwamba nambari ya nchi inaonyesha +61 ambayo ni kwa Australia. Ikiwa unatumia simu ya kimataifa, utapaswa kubadilisha nambari ya nchi kutoka +61 kwa nambari ya nchi ambayo simu yako inatumia.
- Utatumwa msimbo kwa simu yako ya mkononi. Weka msimbo huu kwenye tovuti mahali ambapo panasema ‘passcode’ (msimbo wa siri) halafu bonyeza kifute cha bluu.

KUMBUKA: Ikiwa hii ni mara ya kwanza umetumia Lango mtandaoni la Matokeo, utapaswa kuweka maelezo fulani ya ziada.

- Bonyeza kwa ‘View Results’ (Angalia Matokeo) na utahitaji kuweka:
  - Jina lako la kwanza
  - Jina lako la mwisho
  - Tarehe yako ya kuzaliwa
  - Msimbo wa posta wa nyumbani kwako
  - Jinsia yako – kwa mfano, kiume au kike au kingine
  - Tarehe ya kukusanya – hii ni tarehe uliyopimwa
  - Nambari yako ya Medicare kama unayo. Ikiwa huna nambari acha kuwa tupu.

- Bonyeza kifute bluu kwa sehemu ya juu inayosema, ‘Select collection centre’ (Chagua kituo cha kukusanya) na tafuta kwa mahali ambapo ulipopata kipimo chako cha COVID-19. Pamoja na vituo vinavyoendeshwa na Idara ya Afya ya NSW kuna vituo pia ambavyo vinajitegemea. Ikiwa unachagua kituo ambacho hakiendeshwi na Maabara ya Afya ya NSW, tovuti hii itakupa maelezo kuhusu jinsi ya kuwasiliana na kliniki kupata matokeo yako.
- Ili kuona matokeo yako, bonyeza kwa ‘View Results’ (Angalia Matokeo).
- Utaulizwa kuchapisha jina lako ya kwanza na tarehe yako ya kuzaliwa kama DDMMYYYY, kwa mfano, 01051971.
- Utaweza kupatikana na kupakua nakala ya matokeo yako ya kipimo cha COVID.

**Chaguo la 3: Pokea SMS**
Ikiwa huwezi kupatikana langoni mtandaoni la matokeo, unaweza kupokea matokeo yako kupitia SMS kwa simu yako ya mkononi.

- Tuma maneno ‘my result’ (matokeo yangu) kwa 0480 050 030
- Wakati unapoulizwa, tafadhali tuma SMS na habari zifuatazo:
    - Jina lako la mwisho.
    - Tarehe yako ya kuzaliwa kwa kutumia nambari tu – DDMMYYYY. Kwa mfano, 01012000
    - Ikiwa unaandikisha kwa ajili ya mtoto, utaulizwa kuhakikisha kuwa wewe ni mzazi au mlezi na unaweza kufanya maamuzi ya huduma ya afya kwa ajili kwa mtoto huyo. Tuma ujumbe wa Yes (ndio) ili kuhakikisha.
    - Jinsia yako kuwa M kwa Kiume, F kwa Kike au O kwa Kingine.
    - Msimbo wako wa posta, (kwa mfano 2114)
    - Tarehe ambayo ulipata kipimo chako cha COVID-19 kama DDMMYYYY, kwa mfano, 01052021
- Kagua habari yako na chapisha Yes (ndio) ikiwa ni sahihi. Kama umefanya makosa, chapisha No (Hapana) ili kuanza tena.
- Wakati unapomaliza utapata ujumbe ambao unasema, ***‘Your registration has been* received’ (*Usajili wako* umepokelewa).**
- Utapata pia msimbo wa siri ambao utapaswa kuchapisha ili kupata matokeo yako.
- Wakati ambapo matokeo yako ni tayari utapata ujumbe wa SMS ambao utakuuliza kuchapisha neno la ‘Ready’ (Tayari) pamoja na msimbo wako wa posta.
- Matokeo yale yatakuja kwa simu yako

**Je, unahitaji msaada wowote?**
Ikiwa unapata matatizo ya kupata matokeo yako na imekuwa muda wa zaidi ya masaa 48, unaweza kufuatilia kupitia tovuti yetu kwa https://www.pathology.health.nsw.gov.au/covid-19-info/covid-19-results-direct

**Nini itatokea kama matokeo yangu yanaonyesha kuwa ninayo COVID-19?**
Ikiwa kipimo chako kinaonyesha unayo COVID-19, na umejiandikishwa kupokea matokeo yako kupitia moja ya chaguzi hizi, utapokea SMS inayokuambia kwamba matokeo yako yanapatikana kupitia Lango la Matokeo, pamoja na maelezo zaidi juu ya kujitenga.

Utawasiliana pia na wafanyakazi kutoka timu ya Afya ya Umma ya eneo lako.

**NOTISI YA KUKUSANYA SIRI:** Maabara ya Afya ya NSW (NSWHP) hukusanya habari kwa madhumuni ya kuarifa wagonjwa matokeo yao ya kipimo cha COVID-19. Habari hii itatumiwa kwa kawaida katika Afya ya NSW hata hivyo inaweza pia kufichua kwa ServiceNSW kwa madhumuni ya kuarifa matokeo kwa wagonjwa. Watu binafsi wana haki ya kisheria ya kupata habari ambazo shirika la serikali linashika juu yao. Kwa habari zaidi tembelea www.pathology.health.nsw.gov.au/about-us/privacy. Athari zinazowezekana za watu kutotoa zote, au sehemu, za habari ambazo zinaulizwa zinaweza kutokea na NSWHP kutoweza kutoa matokeo ya vipimo kwa wagonjwa.